



TANGAZO

UUZAJI WA MALIGHAFI ZA MITI KATIKA MASHAMBA 14 YA MITI YA KUPANDA YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utavuna miti laini na migumu katika mashamba 14 ya miti ya kupanda yanayomilikiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027 (Kiambatisho No. 1).

- Mashamba 12 ambayo yapo Sehemu A ya Kiambatisho yatazingatia mambo yafuatayo:-

1. Wamiliki wa viwanda ambao wana nia ya kuendelea na uvunaji wanashauriwa ku wasilisha maombi ya kupatiwa malighafi kwa kujaza fomu ya maombi ya uvunaji wa miti na kuyatuma kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la miti husika.
2. Waombaji wanya wenye sifa zinazotakiwa na wanadhamiria kufanya shughuli za uvunaji wanashauriwa kuwasilisha maombi yao kwenye mashamba yenye mgao wa ziada ikiwemo Ukaguru, Shume, Meru na West Kilimnjaru. Aidha, mashamba ya Meru na West Kilimanjaro inapatikana miti migumu peke yake.
3. Fomu za maombi zinapatikana katika ofisi za wahifadhi wakuu wa mashamba husika na pia katika tovuti ya wakala (www.tfs.go.tz)
4. Mwisho wa kupokea maombi ya uvunaji wa miti ni tarehe 03 Juni, 2026 saa 9:00 alasiri.
5. Mwombaji anapaswa kufika Ofisi za Shamba akiwa na kitambulisho cha Taifa au Leseni ya udereva au Pasi ya kusafiria.
6. Maombi yatakayowasilishwa kwa utaratibu tofauti na maelekezo haya ha-yatashughulikiwa.

- Mashamba 2 ambayo yapo Sehemu B ya Kiambatisho yatazingatia masharti na vigezo vya uuzaji wa miti kwa njia ya mnada wa kielekroniki hivyo wahitaji wa malighafi hiyo wafuatilie matangazo ya minada ambayo hutolewa mara kwa mara katika tovuti ya wakala (www.tfs.go.tz)

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Wakala: www.tfs.go.tz



KIAMBATISHO NO. 1: ANUANI ZA MASHAMBA YA MITI AMBAYO UVUNAJI UTAFAFYIKA

Na.	Jina la Shamba	Anwani	Mahali lilipo	Aina ya miti
SEHEMU A:				
1	Sao Hill	S.L.P 45, Mafinga	Mufindi - Iringa	Misindano (Pinus patula), na Mikaratusi (Eucalyptus spp).
2	Meru/Usa	S.L.P 1257 Arusha	Arumeru - Arusha	Misindano (Pinus patula), Mikaratusi (Eucalyptus maidenii), Mkavelia (Grevillea robusta), na Acacia melanoxylon.
3	Buhindi	S.L.P 1480 Mwanza	Sengerema - Mwanza	Misindano (Pinus caribaea & Pinus tecunumanii).
4	North Kilimanjaro	S.L.P 40 Tarakea	Rombo - Kilimanjaro	Misindano (Pinus patula), Mikaratusi (Eucalyptus spp), Acacia melanoxylon, na Mti kunuka (Cedrela odorata). Grivelia robusta Cupressus lusitanica.
5	West Kilimanjaro	S.L.P 161 Hai	Hai - Kilimanjaro	Misindano (Pinus patula), Mikaratusi (Eucalyptus spp) na Cupressus lusitanica. Grevillea robusta
6	Shume	S.L.P 60 Lushoto	Lushoto - Tanga	Misindano (Pinus patula), Cupressus lusitanica, na Mikaratusi (Eucalyptus spp)
7	Kawetire	S.L.P 770 Mbeya	Mbeya	Misindano (Pinus patula), na Mikaratusi (Eucalyptus maidenii).
8	Kiwira	S.L.P 991 Mbeya	Rungwe - Mbeya	Misindano (Pinus patula)
9	Rubya	S.L.P 134 Nansio	Ukerewe - Mwanza	Misindano (Pinus tecunumanii na Pinus caribaea)
10	Rubare	S.L.P 930 Bukoba	Bukoba - Kagera	Misindano (Pinus caribaea)
11	Ukaguru	S.L.P 2 Gairo	Gairo - Morogoro	Misindano (Pinus patula), na Mikaratusi (Eucalyptus spp).
12	Rondo	S.L.P 205 Rondo	Lindi	Misindano (Pinus caribaea)
SEHEMU B:				
13	Longuza	S.L.P 190 Muheza	Muheza-Tanga	Misaji (Tectona grandis)
14	Mtibwa	S.L.P 18 Turiani	Turiani-Morogoro	Misaji (Tectona grandis)

**Imetolewa na;
KAMISHNA WA UHIFADHI
S.L.P. 2228 DODOMA**

